

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

Simu Na: +255 (026) 2963630
Nukushi: +255 (026) 2963629
Barua Pepe: ps@utumishi.go.tz
Tovuti: <http://www.utumishi.go.tz>



Menejimenti ya Utumishi wa Umma
na Utawala Bora,
Jengo la Taaluma Na. 1,
Chuo cha Masomo ya Biashara na Sheria,
Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),
18 Barabara ya Mkalama,
S.L.P. 670,
40404 DODOMA.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

WAAJIRI WASHAURIWA KUTOA MAFUNZO KWA VIONGOZI WAPYA WA MABARAZA YA WAFANYAKAZI SERIKALINI ILI WAZEWE KUTIMIZA MAJUKUMU YAO IPASAVYO

Wajiri katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekretarieti za mikoa wametakiwa kutoa mafunzo kwa wajumbe na viongozi wapya wa mabaraza ya wafanyakazi ili waweze kumudu majukumu yao ya kusimamia haki za watumishi ipasavyo.

Rai hiyo ilitolewa na Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dkt. Francis Michael wakati wa kikao cha baraza la wafanyakazi la ofisi yake kilichofanyika katika ukumbi wa Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa jijini Dodoma.

Dkt. Michael alisema kuwa, endapo wajiri wataweka utaratibu wa kutoa mafunzo kwa viongozi na wajumbe wa mabaraza mapya ya wafanyakazi, itawawezesha kufahamu majukumu yao vizuri.

Dkt. Michael alifafanua kuwa, lengo la kuwapo kwa mabaraza ya wafanyakazi serikalini ni kujadili hoja za watumishi kupitia wawakilishi katika mabaraza ya wafanyakazi ili kuwapo na maslahi mazuri na pia kuongeza tija katika utendaji kazi wa wafanyakazi.

Naye, Katibu wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bi. Lilian Denis amewataka wawakilishi wa watumishi katika mabaraza ya wafanyakazi kuhakikisha wanawasilisha masuala ya msingi katika mabaraza hayo ili kupatiwa ufumbuzi ambao utaongeza ari ya utendaji kazi ndani ya taasisi husika.

Akizungumza kwa niaba ya wafanyakazi wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bi. Menyiaichi Koka amesema kuwa

uwapo wa mabaraza ya wafanyakazi serikalini utasaidia kuongeza nidhamu ya kazi, kukuza maadili ya utendaji kazi na kuepusha migogoro sehemu za kazi.

Baraza la wafanyakazi la Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora limehudhuriwa na wajumbe wa baraza hilo, Wakuu wa Idara na Vitengo wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na wawakilishi wa TUGHE tawi la Utumishi ambao wamepata fursa ya kujadili mambo yanayohusu ustawi wa watumishi, motisha za watumishi, vitendea kazi, mazingira bora ya kufanya kazi na namna bora ya kuimarisha mahusiano mazuri kazini.

IMETOLEWA NA;
KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
OFISI YA RAIS (UTUMISHI)
TAREHE 16 MACHI, 2019